# Ripoti ya Kiuchumi ya Kenya 2018

## Tafsiri Pendwa

*Kupiga Jeki Uwekezaji kwa Ajili ya Utekelezaji wa Ruwaza ya Kenya 2030*

*Kujenga taifa lenye ushindani na lenye ufanisi kimataifa*

© 2018 Kenya Institute for Public Policy Research and Analysis (KIPPRA)
Bishops Garden Towers, Bishops Road
S. L. P. 56445-00200, Nairobi, Kenya
Simu: +254 20 2719933/4, Fax: +254 20 2719951
Simu tamba: +254 724 256078, 736 712724
Barua pepe: admin@kippra.or.ke
Mtandao: http://www.kippra.org
Twitter: @kipprakenya

**Haki na Idhini**

Toleo hili ni zao la Kenya Institute for Public Policy Research and Analysis (KIPPRA). Yaliyomo katika toleo hili yamelindwa na haki miliki. Kunakili na/au kusambaza sehemu au toleo hili lote pamoja na mazao yake bila ruhusa/idhini kutoka kwa taasisi husika kutachukuliwa kuwa ni uvunjaji wa sheria zilizoko. KIPPRA huhimiza usambazaji wa kazi zake na kwa kawaida, itatoa idhini kwa haraka ili kutumia sehemu za kazi husika. Ili kupata idhini ya kunakili au kutolesha nakala ya kazi hii au hata sehemu zake, tafadhali tuma maombi ukiambatisha habari kamili kwa ***admin@kippra.or.ke***

**ISBN 9966 058 XX X**

# Kupiga Jeki Uwekezaji kwa Ajili ya Utekelezaji wa Ruwaza ya Kenya 2030

## Uthabiti na Ukuaji wa Kiuchumi wa Maeneo Mapana

Licha ya kipindi kirefu cha uchaguzi na madhara ya ukame uliokithiri mwaka wa 2017, uchumi wa Kenya ulibakia kuwa imara na unaoweza kubadilika na kurudia hali yake ya awali kwa urahisi kupitia uimarikaji wa uthabiti wa kiuchumi wa maeneo mapana. Kwa kawaida, mfumko wa gharama za maisha ulibakia katika kiwango kilichotarajiwa na serikali ingawa kulikuwa na ongezeko la gharama za maisha kiasi kutokana na ukame uliokithiri kabla ya mikakagti ya kuuthibiti ukame huo kuwekwa. Ongezeko la matumizi ya serikali kwa ajili ya maendeleo ulipanuka, jambo ambalo lilipelekea serikali kukopa zaidi, lakini kwa kuzingatia matumizi ya pesa kwa busara, tulifanikiwa kuthibiti madeni kiuendelevu kwa muda huo. Salio la akaunti ya hundi lilipungua na kuongezeka kwa pesa zinazotumwa na Wakenya wanaoihsi ng'ambo kulisaidia kupunguza salio la malipo yetu. Kwa sababu hii, masalio yetu ya kigeni yalibakia kuwa juu ya kiwango kinachotakikana kisheria.

Licha ya hayo, ukuaji wa jumla ya pato la nchi (GDP) lilipungua kufikia 4.9% mwaka wa 2017 ikilinganishwa na 5.9% mwaka wa 2016. Ukuaji katika sekta ya kilimo ulipungua kufikia 1.6% lakini ulizidisha mchango wake wa juu (31.5%) wa jumla ya pato la jumla la nchi huku uzalishaji wa sekta ya viwandani wa 0.2% ukidhihirisha kupungua kwa mchango wa sekta hii kwa jumla ya pato la nchi kwa 8.4%. Hali ya uwekezaji ulibakia chini ya kiwango lengwa cha awamu ya pili ya mipango ya maendeleo na hivyo basi kuwa chini ya kiwango kilichotarajiwa ili kuwa na ukuaji wa asilimia kumi na zaidi kama inavodhamiriwa katika ruwaza ya Kenya 2030 kwa kiasi cha 30%. Tofauti kati ya akiba na uwekezaji uliendelea kuwepo kutokana na ukuaji duni wa akiba. Pamoja na hayo, ukuaji mdogo wa mikopo kwa sekta ya kibinafsi uliendelea kwa sababu benki zilikubali kutumia aina mbalimbali

**UTENDAKAZI WA UKUAJI WA KIUCHUMI WA MAENEO PANA NA MATAZAMIO YA UKUAJI**

**WACHANGIAJI WAKUU KATIKA UKUAJI WA KIUCHUMI**

| Sekta | Mchango |
|---|---|
| Malazi na huduma za chakula | 15.0% |
| Habari na mawasiliano | 11.0% |
| Ujenzi | 8.6% |
| Usafiri na maghala | 7.4% |
| Mali isyohamishika | 6.2% |
| Uchimbaji madini na mawe | 6.1% |

**UWEKEZAJI NA AKIBA**

- Kiwango cha uwekezaji kiliongezeka kutoka 21% kufikia 24% wakati wa utekelezaji wa muhula wa wastani awamu ya 1 na ya 2, lakini kilikuwa chini ya kiwango lengwa cha 30%.
- Jumla ya akiba ya nchi ilikuwa baina ya 10% na 13% ya jumla ya pato la nchi
- Thamani ya jumla ya mpango wa fedha halisi ulipungua kwa 9.4% mwaka wa 2016

**UTENDAJI WA KIFEDHA**

- Jumla ya malimbikizo ya mapato, pamoja na misaada ilikuwa shilingi bilioni 1.514.9 mwaka wa 2017/2018 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.426.9 mwaka wa 2016/2017. Hata hivyo, ilikuwa chini ya kiwango kilichotarajiwa cha shilingi bilioni 1.702.6.
- Jumla ya matumizi na ukopeshaji halisi ilikuwa shilingi bilioni 2.111.5 mwaka wa 2017/2018 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.109.0 mwaka wa 2016/2017. Lengo lilikuwa shilingi bilioni 2.330.0.
- Hasara ya fedha halisi inayokusanywa iliimarika kufikia kiwango cha shilingi bilioni 596.6 mwaka wa 2017/2018 ikilinganishwa na shilingi bilioni 697.3 iliyokusanywa mwaka wa 2016/2017.
- Hata hivyo hasara hii ya fedha halisi iliyokusanywa ilikuwa chini ya kiwango kilichotarajiwa cha shilingi bilioni 627.4 kutokana na mapato halisi kutotimiza malengo yaliyowekwa na viwango vya chini vya matumizi ya bajeti ya matumizi vilivyorekodiwa.

**DENI LA UMMA**

- Liliongezeka hadi 57.2% ya jumla ya pato la nchi mwaka wa 2016/2017 kutoka 55.5% mwaka wa 2015/2016.
- Kutokana na ongezeko la uwekezaji wa umma uliogharamiwa kutoka nje.
- Kufikia Disemba 2017, jumla ya muamana ilikuwa inaongezeka kwa 7.6% ikilinganishwa na 6.4% Disemba 2016.

**MABAKI KATIKA AKAUNTI YA HUNDI**

- Iliongezeka kufikia 6.7% ya jumla ya pato la nchi mwaka wa 2017 ikilinganishwa na 5.1% mwaka wa 2016.
- Jumla ya mauzo nchi za nje iliongezeka kutoka shilingi bilioni 578.1 mwaka wa 2016 kufikia shilingi bilioni 594.1 mwaka wa 2017.
- Mabaki ya jumla ya malipo iliongezeka na kufikia nakisi ya shilingi bilioni 169 kutoka salio la shilingi bilioni 13.1 mwaka wa 2016.

za biashara ili kukabiliana na hatari kubwa za uwekezaji baada ya kuanzishwa kwa viwango vya juu vya utozaji riba Septemba 2016.

Katika kipindi cha wastani, serikali inalenga utekelezaji wa ajenda kuu nne na kumalizia uwekezaji ulioanzishwa katika kipindi cha wastani cha muhula wa pili. Hii inatarajiwa kuendelea kupanua uwezo wa shughuli za kiuchumi na wakati huo huo ikithibitishwa kuwa ukuaji uliopatikana ni jumlishi katika kuinua hali ya maisha ya wanajamii. Kwa sababu hii, mikakati ya kati yenye ubora na ufaafu inahitajika ili kudumisha msukumo wa maendeleo.

Uthabiti wa kifedha ungali ukipewa kipaumbele ili kudumisha uthabiti wa kiuchumi wa maeneo mapana. Kwa kuwa sera ya kifedha itaendelea kuchangia pakubwa ukuaji wa kiuchumi, ni sharti tuhakikishe kuwa sera zinazoendeleza ukuaji wa kiuchumi zitaendelea kudumisha mkondo wa ukuaji wa kifedha. Zaidi ya hayo, kuzidisha usimamizi wa madeni ufaao kutasaidia kudumisha madeni endelevu.

Ili kuharakisha ukuaji wa uwekezaji, ni muhimu kuhamasisha rasilmali za humu nchini. Hili litawezekana kwa kutumia nafasi zilizoko ili kuongezea mapato, kuhimiza uwekaji akiba wa kibinafsi kupitia ukuzaji wa sekta ya kifedha kwa kuimarisha asasi


za maendeleo ya kifedha zilizoko. Pamoja na hayo, ni muhimu kuimarisha mfumo wa asasi na usimamizi kati ya mawakala wa kitaifa na serikali za kaunti ili kuendeleza uwekezaji wa moja kwa moja kutoka ugenini ambao ni njia ifaayo ya kugharamia miradi bila mikopo. Muhimu zaidi, sera ya kifedha yenye kuhimili na uthabiti wa kiuchumi vitazidisha imani ya soko.

## Kupiga Jeki Ukuaji wa Sekta ya Uzalishaji Viwandani

Sekta ya uzalishaji viwandani ina uwezo mkubwa wa kusaidia ajenda ya maendeleo hususan kwa kuongezea thamani na kupanua vianzo vya ukuaji. Pamoja na ajenda kuu nne, sekta hii inatarajiwa kuchangia angalau 15% ya pato la jumla la nchi kufikia mwaka wa 2022, msisitizo ukiwa katika sekta ndogo za utengenezaji wa bidhaa za kilimo, nguo, ngozi na uchumi wa majini. Ili kufanikiwa kufikia lengo hili, sekta hii inatakiwa kuzidisha uzalishaji wake maradufu kutoka viwango vya sasa.

Kipengele muhimu cha kuharakisha ukuaji wa sekta ya uzalishaji viwandani ni kuboresha ushindani wa viwanda. Hii inamaanisha ujenzi wa muundo tata zaidi wa bidhaa zinazotolewa ulio na uwezo ulioimarika ili kuweza kuzalisha bidhaa kwa kutumia teknolojia ya kisasa hususan kupitia ubadilisho wa kiteknolojia na mafunzo ya kiufundi. Pamoja na hayo, kuna haja ya kuharakisha ujenzi wa maeneo muhimu ya kiuchumi yaliyolengwa ili kuweza kuwavutia wawekezaji, ikiwemo utaratibu imara






na serikali za kaunti ili kuhakikisha kuwa ardhi ya kutosha inatengewa maeneo hayo. Mbali na hayo, ili kuzuia ushindani usiofaa katika soko la humu nchini, ni muhimu kurejelea na kutathmini vivutio vinavyotolewa kwa makampuni yaliyo katika maeneo haya dhidi ya yale yanayoendesha shughuli zao nje ya maeneo hayo.

Ili kuunga mkono ukuaji, ukomavu na uhitimu wa biashara ndogo na za wastani na kuharakisha upatikanaji wa teknolojia, fedha na uvumbuzi, kuna haja ya; kwanza, kubainisha na kulea taratibu za kupata kandarasi ndogondogo kwa ushirikiano na makampuni makubwa. Pili, kuna haja ya kuelekeza juhudi zetu kwa matendo ya kuendeleza biashara katika sera za biashara ndogondogo na za wastani ili ziweze kushiriki katika uongezeaji thamani kiwango cha eneo hili na kimataifa. Tatu, utekelezaji unaofaa wa sheria na kanuni za ununuzi zilizoko kuhusiana an matumizi ya rasilmali ya humu nchini, na nadhari maalum kwa kina mama na vijana, vinaweza kuharakisha ukuaji wa biashara ndogondogo na za wastani. Nne, utekelezaji unaofaa

wa sera ya bidhaa ghushi unahitajika ili kupunguza uingizaji wa bidhaa za hali duni na kulinda makampuni ya humu nchini kutokana na ushindani usiofaa.

Mwisho, kuimarisha asasi kama vile Kenya Industrial Estates (KIE), Kenya Industrial Research Development Institute (KIRDI), na Kenya Intellectual Property Institute (KIPI) ni muhimu ili kujenga utamaduni wa viwanda na kuzidisha ushindani katika biashara ndogondogo na za wastani. Aidha, uboreshaji wa kudumu wa mazingira ya kufanyia biashara katika viwango vya kaunti na serikali kuu kutasaidia kusukuma maendeleo ya viwandani.

## Kuchochea Uwekezaji Katika Biashara

Biashara huchangia pakubwa mabadiliko ya kiuchumi kwa kuongezea uzalishaji, kuongezea ubadilishanaji wa mawazo na uvumbuzi, kuongezea upatikanaji wa aina nyingi zaidi wa bidhaa kupitia mchakato wa usambazaji na kutoa nafasi za ajira. Kwa hivyo, ukuaji na maendeleo ya kibiashara ni muhimu katika kusaidia utekelezaji wa "Ajenda Nne Kuu".

Biashara za rejareja na za jumla humu nchini huajiri 60% ya wafanyikazi katika sekta isiyo rasmi na zimepata upenyo wa kiasi cha juu kupitia uboreshaji wa jumla wa mazingira ya kuendeshea biashara. Hata hivyo, wingi wa malipo, ada, na kodi zinazotozwa wafanyibiashara na serikali kuu na zile za kaunti huongezea gharama za kufanyia biashara na kupinga uwekezaji katika sekta zalishi za uchumi wa nchi. Mbali na hayo, kuchelewesha utekelezaji wa miradi mikuu ya kipaumbele iliyolengwa kumesababisha upungufu wa masoko ya rejereja na hivyo basi, kuzuia utendaji bora, uletaji wa matokeo yanayotarajiwa, na ukuaji wa usambazaji wa bidhaa na huduma humu nchini.

Katika kiwango cha biashara ya kimataifa, kumekuwa na ongezeko lenye maana katika uingizaji wa bidhaa ambazo zingeweza kuundiwa humu nchini na kusaidia

> ***"Biashara za jumla na za rejareja huwaajiri 60% ya wafanyikazi wa sekta isiyo rasmi. Huku biashara ya jumla na ya rejareja ya humu nchini ikiwa imepata kiwango kikubwa cha upenyo, wingi wa malipo, ada na karo zinazotozwa wafanyibiashara, na serikali ya taifa na zile za kaunti huongezea gharama za kufanyia biashara na kukinga uwekezaji katika sekta zingine zinazofaidi uchumi."***
>
> ***Ripoti ya kiuchumi ya Kenya 2018***



- Kuboresha mazingira ya kufanyia biashara ndani ya nchi.
- Kuhimiza uongezeaji thamani wa mazao.
- Kupanua masoko ya eneo na ya kimataifa.
- Kuelekeza juhudi za maeneo maalum ya kiuchumi katika mikufu ya masoko ya ndani ya nchi, ya eneo hili, na ya kimataifa.
- Kuimarisha muungano wa kiuchumi kati ya uchumi wa Kenya na nchi jirani.

uzalishaji wa humu nchini ikiwemo uzalishaji katika viwanda vya nguo na ngozi. Uungaji mkono upanuzi wa maeneo maalum ya kiuchumi na kuimarisha ari ya nunua Kenya jenga Kenya huku tukihakikisha upatanisho katika utekelezaji wa sera ya kitaifa ya biashara na mkakati wa ujenzi wa viwanda utahimiza matumizi ya bidhaa za humu nchini, uongezeaji thamani, na kuongezea mbinu za uzalishaji. Mbali na hayo, ushirikiano hai wa Kenya katika masuala ya muungano wa kiuchumi wa eneo na utekelezaji wa mipango mbalimbali ya kuharakisha biashara umekuwa na umuhimu mkubwa katika kuimarisha mazingira ya kufanyia biashara na kusaidia upatikanaji wa masoko katika eneo hili na kimataifa. Tukiangazia mbele, Kenya



> Katika kiwango cha biashara ya kimataifa, kumekuwa na ongezeko lenye manufaa katika uingizaji wa bidhaa kutoka nje ambazo zingetengenezewa humu nchini ili kusaidia utengenezaji bidhaa mumu humu nchini ikiwa ni pamoja na viwanda vya kutengeneza nguo na ngozi.
>
> ***Ripoti ya kiuchumi ya Kenya 2018***

inahitaji kuanzisha mkakati wa kutumia kikamilifu uwezo wa soko katika mkataba wa biashara huru katika bara la Afrika (ACFTA) uliokamilika hivi majuzi.

Makampuni yaliyoko maeneo ya kiuchumi yametawaliwa na sekta ndogo za utengenezaji wa bidhaa za nguo, za mashambani na huduma licha ya uwezo wazo wa kuongezea thamani na kutumia wafanyikazi kwa wingi, hutumia viwango vidogo vya malighafi ya humu nchini. Ili kuongezea mapato ya mauzo ya nje ya nchi na kupanua bidhaa zinazouzwa nchi za nje, kuna haja ya kuzidisha uwezo wa kuongezea thamani bidhaa za kuuza nje kama vile chai, kahawa, na mboga na matunda, wakati tunapokuza utengenezaji wa bidhaa zenye utata wa hali ya juu zaidi. Utekelezaji wa mipango mbalimbali ya kuharakisha biashara umeinua biashara na kusaidia upatikanaji wa masoko ya eneo na ya kimataifa lakini muungano wa makampuni ya humu nchini ili kuongezea thamani ungali chini mno. Kwa kuanzia, kuna haja ya kuhimiza ushirikiano wa biashara ndogondogo na za wastani katika mkufu wa usambazaji bidhaa, kuhimiza utumiaji wa mali ghafi ya humu nchini kwa kuhimiza maunganisho ya kandarasi ndogondogo kwa kushirikiana na makampuni makubwa na kutumia kikamilifu nafasi za ununuzi zinazopatikana serikalini.

Wakati Kenya imetia sahihi mapatano ya uwekezaji kati ya nchi mbili na mataifa mbalimbali ili kuimarisha na kusaidia uwekezaji wa kigeni, uratibu kati ya mawakala wa serikali kuu na zile za kaunti kwa utekelezaji unaofaa umekuwa haupo. Licha ya hayo, sera ya uwekezaji inahitaji kufungamanishwa upya na mikakati ya maendeleo ya dijitali ili kuwezesha makampuni ya humu nchini kufaidika kwa hali hiyo kutokana na udijitali na upatikanaji wa haraka wa masoko ulimwenguni.

## Kuwekeza ili kukuza sekta ya utalii

Utalii humu nchini una uwezo wa kuchangia kwa jumla ya pato la nchi, mapato ya fedha za kigeni, ajira na kuzalisha pato. Kuhusu suala hili, miradi mikuu ya

- Kenya huvutia idadi kubwa zaidi ya watalii kutoka nje katika jumuiya ya Afrika Mashariki
- Utalii huchangia 10% ya pato la jumla la nchi kila mwaka.
- Huchangia karibu 3.5% kwa ajira za moja kwa moja na 9.0% kwa ajira zisizo za moja kwa moja
- Kiwango cha mapato ya utalii na watalii waliokuja huku mwaka wa 2017 kiliongezeka kwa 20.3% na 8.1 mtawalia

Malengo ya watalii wanaofika Kenya kufikia 2030 ni milioni 30.4

Ajira za moja kwa moja 561,800

Ukuzaji wa bidhaa; uuzaji; muundomsingi; utangazaji wa uwekezaji katika utalii





> Katika eneo la Afrika Mashariki, Kenya ina idadi kubwa zaidi ya watalii kutoka nje kila mwaka. Hata hivyo, nchi hii inapata ushindani mkubwa kutoka Tanzania. Wakati kuinukia kwa sekta ya utalii kulizidishwa mwaka wa 2017, sekta hii ingali ikipata ushindani mkubwa ikilinganishwa na sehemu zingine za kitalii kama vile Afrika Kusini katika viwango vya idadi ya watalii, mapato na tajriba anuwai.
>
> ***Ripoti ya kiuchumi ya Kenya 2018***

kipaumbele mbalimbali ilitambuliwa ili kuimarisha maendeleo na ustawi wa sekta hii lakini baadhi ya miradi hii ingali kukamilishwa. Katika kiwango cha kaunti, ustawi wa utalii unahitaji kutengewa pesa za kutosha katika bajeti ili kuiwezesha kutumia kikamilifu nafasi za utalii wa kitamaduni na kiubunifu. Wakati idadi ya watalii wanaokuja hapa nchini inaongezeka huku serikali ikiingilia kati kuimarisha usalama, matumizi ya hoteli na wageni imepungua huku wageni hao wakipendelea kutumia vifaa mbadala vya malazi. Ili kuendelea kuinua ushindani wa Kenya kama mahali panapofaa zaidi kwa utalii, uwekezaji wenye maana unahitajika katika kuendeleza muundomsingi unaoambatana na shughuli za utalii. Kwa hivyo, kutokana na ufadhili kidogo wa miradi mikubwa, ni sharti ufadhili mbadala utafutwe.

Kumeshuhudiwa uwekezaji mpya hususan katika utoaji wa vifaa vya malazi, na kuna nafasi nyingi sana za kuwekeza katika miradi mikubwa ya kiutalii inayohusisha ushirikiano kati ya umma na makampuni ya kibinafsi katika nyanja za ujenzi wa muundomsingi unaoambatana na shughuli za utalii katika viwango vya serikali kuu na zile za kaunti, ikiwemo viwanja vya ndege, vifaa vya M.I.C.E., na vifaa vya malazi na michezo. Katika kiwango cha kitaifa, miradi mikuu ya kipaumbele iliyotambuliwa ili kuhimiza ukuaji na maendeleo ya sekta hiyo ingali bado kukamilishwa. Licha ya hayo, serikali za kaunti zingali bado kutumia nafasi zilizoko kikamilifu katika utalii wa kitamaduni na kiubunifu.

## Kuzidisha Utoshelevu wa Chakula kwa Uwekezaji Zaidi Katika Kilimo

Kilimo ni muhimu sana kwa utoshelevu wa chakula, maendeleo ya mashambani, na mabadiliko ya kiviwanda. Ukuaji wa kilimo unafaa zaidi katika kupunguza umaskini ikilinganishwa na ukuaji wa sekta nyingine yoyote kwa sababu ya idadi

> ...hali ambayo watu wote, kila mara wana upatikanaji wa kutosha kimwili na kiuchumi chakula cha kutosha, salama, na chenye lishe ili kukabili mahitaji yao ya lishe na mapendeleo yao ya chakula kwa ajili ya maisha hai na yenye afya nzuri.
>
> ***Ripoti ya kiuchumi ya Kenya 2018***




kubwa ya watu wanaotegemea sekta hii moja kwa moja. Kutokana na hilo, sekta hii ni muhimu katika kufanikisha malengo ya ruwaza ya 2030, kuhakikisha utoshelevu wa chakula kama inavyoelezewa katika ajenda kuu nne, na kuondolea mbali njaa kama ilivyoelezewa katika kifungu 43(1) cha katika ya Kenya.

Ili kufanikisha utoshelevu wa chakula, ni muhimu kupunguza hasara za baada ya kuvuna. Kiwango cha wastani cha hasara za baada ya kuvuna upande wa mahindi ambayo ndiyo chakula muhimu nchini Kenya ni 21%, kwa wingi kutokana na uzembe katika utunzaji wa mahindi, uhifadhi usiofaa, na ukosefu wa maarifa ya teknolojia za uhifadhi katika mkufu wa thamani wa chakula. Uongezeaji thamani duni katika kilimo pia huchangia hasara kubwa baada ya mavuno. Hivyo basi kuongezea uhaba wa chakula.

Kutegemea zaidi mvua katika mfumo wa uzalishaji wa kilimo unabakia kuwa changamoto katika uzalishaji mashambani. Hii inahitaji nchi kuhimiza kwa wingi

> Sekta ya kilimo inatawaliwa na wakulima wadogowadogo wanaomiliki chini ya ekari tano (5) za shamba kila mmoja lakini wanazalisha 75% ya mifugo, chakula cha kuliwa nyumbani na cha kuuzwa humu nchini, na 73% ya mazao huuzwa katika soko la humu nchini.
>
> ***Ripoti ya kiuchumi ya Kenya 2018***

unyunyiziaji maji mashamba na kutumia kilimo kisichotegemea mvua ili kupunguza madhara ya kudhurika na hali ya anga. Kupunguza gharama za uzalishaji wa kilimo na kutoa huduma za nyanjani ili kuboresha mbinu za uzalishaji kutaongezea mazao ya kilimo.

Pamoja na hayo, kuzidisha utendaji wa asasi muhimu zinazohimili sekta ya kilimo kama vile National Cereals and Produce Board (NCPB), Kenya Meat Commission (KMC), Agricultural Finance Corporation (AFC), na Kenya Dairy Board (KDB) pamoja na kuondoa vikwazo vilivyoezekwa katika mipaka ya kaunti kutaongezea uongezeaji thamani, kupunguza hasara baada ya mavuno, na kuzidisha usambazaji kwa wakati unaofaa kote nchini. Kama shughuli iliyogatuliwa, mtazamo ulio sawa katika kiwango cha serikali kuu na zile za kaunti, miradi ya kilimo inayopewa kipaumbele na yenye ufanisi inahitaji kutekelezwa.

Mbali na hayo, kuongezea aina tofauti za chakula kwa, tuseme, kutumia kikamilifu uwezo wa samaki na uchumi wa majini kutaleta maendeleo katika kufanikisha kiwango cha utoshelevu wa chakula na chenye lishe bora. Ili kufanikisha jambo hili, matumizi ya umma katika serikali kuu na zile za kaunti yanapaswa kuendelezwa kufikia kiwango lengwa cha 10% kilichopendekezwa katika mradi mpana wa ukuzaji wa kilimo barani Afrika (CAADP).

## Kuziba Mianya ya Muundomsingi ili Kupanua Uwezo wa Kiuchumi

Maendeleo ya muundomsingi hupanua uwezo wa kukuza juhudi za kiuchumi, hupunguza gharama za kufanyia biashara, kuwezesha kuinuliwa kwa viwango vya hali ya maisha ya watumiaji, na kuongezea uzalishaji. Ruwaza ya 2030 inadhamiria kujenga vifaa vya usafiri vya kiwango cha kimataifa na vya bei nafuu hususan katika usafiri, nishati, mawasiliano, ujenzi wa nyumba, maji na uondoaji maji taka kwa gharama nafuu.

Wakati muundomsingi nchini Kenya umeimarika katika mwongo uliopita, bado kungali na mianya kiasi. Katika ajenda kuu nne, serikali inadhamiria kubuni wamiliki wa nyumba mpya 500,000 kufikia mwaka 2022 chini ya mpango wa ujenzi wa nyumba zinazomudika pamoja na kumaliza ujenzi wa miradi mikuu ya kipaumbele chini ya ruwaza ya Kenya 2030.



- Sekta ya muundomsingi huchangia 24% ya jumla ya pato la nchi.
- Inawezesha uzalishaji katika sekta zingine.
- Ilichangia 15.5% ya jumla ya ajira mwaka 2017.
- Karibu nafasi 410,500 za ajira rasmi zilibuniwa katika sekta ya umma na ile ya kibinafsi.

Kutokana na uwekezaji wa kiwango cha juu unaohitajika ili kukamilisha miradi ya muundomsingi ya kipaumbele kwa wakati unaofaa, kunahitajika mkakati imara wa kuhamasisha rasilmali ili kutumia ipasavyo nafasi zilizoko humu nchini na kimataifa. Pamoja na hayo, muunganisho wa mipango ya uwekezaji utasaidia kuleta usawa katika ujenzi wa muundomsingi na kuzuia uharibifu wa mali. Zaidi ya hayo, viwango vya juu vya ushirikiano vitahitajika ili kusaidia serikali ya kitaifa na zile za kaunti kutoa mchango wao.

Kuongezea uwezeshaji katika miradi ya maendeleo na usimamizi wake ni muhimu ili kuhakikisha ugavi ufaao na wa kutosha wa huduma zinazohitajika. Pamoja na hayo, kuwekeza katika urekebishaji wa kila mara kutasaidia kudumisha huduma za muundomsingi wa hali ya juu na kupunguza gharama za kujenga muundomsingi mpya siku za baadaye. Mbali na hayo, mfumo wa kulipisha huduma mbalimbali unahitaji kuangaliwa upya ili kupunguza gharama na kuvutia mahitaji ya huduma za muundomsingi.

Mradi wa ujenzi wa nyumba zinazomudika chini ya ajenda kuu nne unahitaji kulengwa ipasavyo ili ijulikane ni nani watakaonufaika na jinsi watakavyotambuliwa na maelezo mafupi (yao) kutolewa. Aidha, kuimarisha usimamizi wa data kutaharakisha upangaji wa majukumu yanayotekelezwa na wahusika mbalimbali katika sekta hii ikiwa ni pamoja na wafafadhiliwa wao lengwa.

Pia kuna haja ya kutumia tecknolojia za ujenzi wa nyumba ambazo zitahifadhi mazingira huku zikipugnuza gharama za ujenzi, kuunda benki za mashamba, na kuimarisha mbinu za usimamizi. Zaidi ya hayo, kuhimiza ushirikiano wa umma na watu binafsi na kutoa vivutio vitakavyosaidia mabenki, vyama vya ushirika



- Sekta zinazotengewa zaidi ya 12% ya jumla ya bajeti ya maendeleo kila mara.
- Jumla ya uwekezaji uliongezeka kutoka shilingi milioni 197 mwaka wa 2008/2009 na kufikia shilingi milioni 600 mwaka wa 2016/2017.
- Mgawo wa bajeti katika kiwango cha kaunti uliongezeka kutoka 6.6% mwaka wa 2013/2014 na kufikia 30.6% mwaka wa 2016/2017.
- Sekta za afya na elimu zilipata kiwango kikubwa zaidi cha ugavi wa uwekezaji.




vya akiba, mashirika ya pensheni, bima, na fedha zitokazo kwa Wakenya walioko nje ni muhimu katika kuhamasisha rasilmali za kugharamia ujenzi wa nyumba zinazomudika.

## Kuwekeza Katika Uwezeshaji wa Mtaji wa Kibinadamu

Uwekezaji katika sekta za kijamii na kiuchumi hujikita katika ustawishaji wa binadamu na uhifadhi wa maskini na walio katika hatari ya kudhuriwa, ambao ni muhimu kwa ukuaji endelevu unaohusisha kila mtu.

**Afya:** Kumekuwa na ongezeko la matumizi ya huduma za afya, jambo lililopelekea matokeo mazuri ya afya. Idadi ya vituo vya afya imeongezeka lakini utoaji wa wahudumu wa afya wanaohitajika imekuwa changamoto. Kutokana na usimamizi mbaya wa rasilmali za afya, kuna nafasi nyingi katika vituo vingi vya afya, ijapokuwa kuna wahudumu wa afya wengi waliofuzu na ambao hawajaajiriwa.

Ili kufanikisha utoaji wa huduma za afya kwa watu wote, serikali inapanua bima ya afya kupitia shirika la NHIF ili kupunguza malipo ya moja kwa moja. Hata hivyo, ili kukidhi mahitaji ya kifedha ya sekta hii kikamilifu, sekta ya kibinafsi inapaswa kushawishiwa kujiunga ili kuzidisha upenyaji wa bima hususan katika sekta isiyo rasmi. Aidha, kupatikana kwa suluhu la migomo ya kila mara ya wafanyikazi wa afya ni muhimu kwa utoaji huduma za afya unaofaa. Kutokana na changamoto zinazoibuka za magonjwa yasiyosambazika, kunahitajika ushirikiano baina ya serikali kuu na serikali za kaunti ili kuhakikisha vituo vya afya vina wahudumu wa afya waliohitimu katika nyanja zao, bidhaa na vifaa vya afya. Pamoja na hayo, kuzidisha upatikanaji wa huduma za afya huhitaji utoaji wa mipango ya afya ya kutosha ili kuzidisha utoaji wa huduma. Kadhalika tunahitaji kutilia maanani zaidi huduma za afya zinazolenga kuzuia magonjwa.

**Elimu:** Katiba ya Kenya inatoa elimu ya bure na ya lazima katika shule za msingi. Ili kufanikisha jambo hili, sekta ya elimu imeshuhudia marekebisho yenye maana mara kwa mara kuanzia marekebisho ya mtalaa wa hivi karibuni, kuanzishwa kwa elimu ya msingi bila malipo, na elimu bila malipo katika shule za upili zisizo za malazi, kufufua taasisi za masomo ya kiufundi, na juhudi zinazoendelea za kuanzisha vituo vya kutoa mafunzo bora katika kila kaunti. Jambo hili limeongezea viwango vya usajili wa wanafunzi na kumaliza masomo katika viwango vyote kuanzia shule za chekechea hadi kiwango cha sekondari, pamoja na taasisi za masomo ya kiufundi.

Pamoja na hayo, idadi ya vifaa vya shule imeongezeka. Wakati elimu ya bure katika shule za msingi na katika shule za upili zisizo za malazi inalenga kuwapunguzia mzigo wazazi, bajeti ya kugharamia elimu imekuwa changamoto. Aidha, ruzuku maalum kwa kila mwanafunzi haitoshi kukidhi mahitaji ya elimu ya kila mmoja wao. Kadhalika, migomo ya kila mara ya wafanyikazi huathiri misimu ya masomo na ukamilishaji wa masomo kama ilivyopangwa.

**Ulinzi wa Jamii:** Mipango ya ulinzi wa jamii imeongezeka kwa kuhakikisha kuwa wanaonufaika wanafikiwa. Hata hivyo, ili kuhakikisha kuwa rasilmali inatumiwa ipasavyo, inahitajika kuwe na uratibu baina ya wahusika wote ikiwa ni pamoja na

kutenga fedha za kutosha ili kuhifadhi faida iliyokwisha kupatikana. Zaidi ya hayo, mpango unaofaa wa kusimamia na kutathmini utasaidia uratibu wa wahusika wote wanaoilinda jamii na kuhakikisha kuwa kuna usalama wa jamii wa kutosha, unaofaa na wenye ufanisi.

## Kuratibu Ukuaji Katika Uwekezaji

Ubora wa mfumo wa asasi ni muhimu katika kukuza uwekezaji. Serikali imeanzisha mageuzi mengi ili kushughulikia vikwazo vya maendeleo katika uwekezaji. Hata hivyo, tunahitaji kuongeza nguvu na kuhakikisha kuwa mageuzi yanaboreshwa ili kushughulikia ushindani daima hususan katika usimamizi wa mali ya umma. Katika juhudi za kushughulikia usawa katika maeneo mbalimbali, serikali imetumia njia ya kuvutia vitega uchumi katika maeneo mbalimbali ingawa tunahitaji mfumo wa uratibu kati ya serikali kuu na zile za kaunti kwa kutilia maanani mfumo wa ugatuzi wa serikali. Jambo hili ni muhimu katika kuzidisha utaratibu wa sera na kurazinisha mfumo wa kanuni katika kiwango cha kitaifa na kaunti.

Wakati Kenya inashiriki katika miradi inayolenga kuleta muungano wa jumuiya ya Afrika Mashariki, ni bora kuimarisha ushirikiano wa nchi wanachama katika kuwekeza katika mataifa mbalimbali. Mbali na hayo, kukuza ushirikiano baina ya nchi za jumuiya ya Afrika Mashariki na mikataba ya kibiashara katika eneo hili kutaharakisha utekelezaji wa miradi iliyopangwa.

Wakati huo huo, kuoanisha kanuni na taratibu kutasaidia utumiaji wa nafasi zilizoko ili kukuza uzalishaji viwandani na uwekezaji kwa maendeleo endelevu.

## Mapendekezo

### Uthabiti na ukuaji wa uchumi wa maeneo mapana

Ili Kenya iweze kukua kwa asilimia kumi na Zaidi, ni sharti uthabiti wa kiuchumi upewe kipaumbele. Kwa sababu hii, nchi inahitaji:

- Kuhakikisha kuwa sera za ukuzaji wa fedha unadumisha mkondo wa kuimarisha fedha nao usimamizi wa deni unazidishwa ili kuhakikisha kuwa deni liko katika kiwango kinachowezekana na kusaidia sera ya fedha kudumishwa ili kupata imani ya soko.

- Kuhamasisha matumizi ya rasilmali za humu nchini kugharamia uwekezaji unaodhamiriwa kwa kutumia nafasi zilizoko za kuongezea mapato ya fedha, kuimarisha mashirika yaliyoko ya maendeleo ya kifedha, kupanua vianzo mbadala vya fedha, na kuimarisha sekta ya kibinafsi ya uwekaji akiba kwa kuimarisha ukuaji wa sekta ya kifedha.

## Kuimarisha ukuaji wa sekta ya uzalishaji viwandani

Ili kuleta mabadiliko katika sekta ya uzalishaji viwandani na kuimarisha mchango wake katika ukuaji wa kiuchumi, kuna haja ya:

- Kuharakisha kukamilishwa kwa ujenzi wa maeneo maalum ya kiuchumi na kuimarisha usimamizi katika viwango vya serikali kuu na za kaunti ili kuharakisha kutambuliwa kwa maeneo yanayofaa katika ujenzi na upanuzi wa maeneo maalum ya kiuchumi katika kaunti zote.
- Kujenga uwezo unaohitajika hasa katika masomo ya kiufundi ili kwendana na uvumbuzi na mabadiliko ya kiteknolojia.
- Kukuza utoaji wa kandarasi ndogondogo na makampuni makubwa kwa biashara ndogo na za wastani ili kuzidisha upatikanaji wa teknolojia, fedha, na uvumbuzi.
- Kuelekeza juhudi zetu za kukuza biashara katika sera za biashara ndogondogo na za wastani ili kusaidia kushiriki kwazo katika uongezeaji thamani wa kieneo na wa kimataifa.
- Kutekeleza ipasavyo sera ya bidhaa ghushi ili kupunguza uingizaji wa bidhaa zisizotimiza viwango vya ubora nchini na kulinda viwanda vya humu nchini kutokana na ushindani usiofaa.
- Kuimarisha asasi kama vile KIE, KIRDI, na KIPI ili kuwezesha ushindani kati ya biashara ndogondogo na za wastani.

## Kukuza uwekezaji kupitia biashara

Ili kuendeleza ukuaji na maendeleo ya biashara, ni muhimu:

- Kuimarisha usimamizi katika kutekeleza mkakati wa uzalishaji viwandani na sera ya kitaifa ya biashara ili kutumia nafasi zilizoko katika kuongezea thamani bidhaa zinazouzwa nje ya nchi na sehemu za mpakani.

- Kuweka mikakati ili Kenya iweze kujinufaisha na uwezo wa soko linalotokana na mkataba wa ACFTA uliofikiwa hivi majuzi na ambao una jumla ya watu wapatao bilioni 1.2 pamoja na jumla ya pato la nchi la US$ trilioni 3.4.
- Kuangalia upya na kurazinisha vivutio vinavyotolewa kwa makampuni yanayoendesha shughuli zao katika maeneo maalum ya kiuchumi dhidi ya yale yanayopatikana katika maeneo yaliyo nje ya maeneo haya ili kuepuka ushindani usiofaa katika soko la humu nchini.
- Kuunda mfumo wa usimamizi kati ya mashirika ya kitaifa na serikali za kaunti ili kukuza na kulenga uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje.

## Kuwekeza Ili Kukuza Sekta ya Utalii

Ili kuendeleza ushindani wa Kenya kama nchi inayowavutia watalii kwa wingi, kuna haja ya:

- Kukamilisha miradi mikubwa ya kipaumbele ya utalii iliyotambuliwa ili kuifanya nchi kuwa eneo lenye ushindani mkubwa wa utalii.
- Kukuza bidhaa mpya zikiwemo utalii wa kiutamaduni na wa kiubunifu katika kaunti zote.
- Kutekeleza sera ya kutoa visa kwa wageni wanaozuru nchi yetu wanapoingia nchini ili kunufaika kutokana na uthibitisho wa mkataba wa SAATM unaohusiana na anga wazi.
- Kuoanisha mafunzo ya utalii na mahitaji ibuka ya sekta hii.
- Kuchunguza kuwepo kwa nafasi za ubunifu zilizoko za uwekezaji wa muda mrefu katika shughuli zinazohusiana na utalii ikiwemo ushirikiano kati ya mashirika ya umma na makampuni ya watu binafsi.
- Kuongezea uwezo wa mashirika ya umma yaliyoko na yenye mamlaka ya kukuza sekta hii.

## Kuzidisha utoshelevu wa chakula kwa kuongezea uwekezaji katika kilimo

Ili kuimarisha uzalishaji wa kilimo ili kujitosheleza kwa chakula, kuna haja ya:

- Kufufua huduma za nyanjani na kutumia njia endelevu ili kupunguza gharama za pembejeo za mashambani hasa mbegu na mbolea.

- Kuanza kutumia kilimo kisichotegemea mvua ili kupunguza hasara ya kilimo kutokana na hatari za anga.
- Kuimarisha asasi katika mkufu wa kuongezea thamani ili kuzidisha uzalishaji na kupunguza hasara baada ya mavuno.
- Kuanza kutumia mtazamo angavu katika kiwango cha kitaifa na serikali za kaunti kwa utekelezaji unaofaa wa miradi ya kilimo.

## Kuziba mianya ya muundomsingi ili kupanua uwezo wa kiuchumi

Ili kudumisha msukumo wa ujenzi wa muundomsingi, kuna haja ya:

- Kuanzisha mkakati imara wa kuhamasisha rasilmali ili kuhakikisha kuna fedha za kutosha kujenga miradi ya muundomsingi na kuanza kutumia mpango wa uwekezaji ulio sawa kwa matumizi bora ya rasilmali.
- Kujenga uwezo katika mpangilio na usimamizi wa miradi.
- Kuwekeza katika urekebishaji ili kuhakikisha ubora wa huduma za muundomsingi na kupunguza gharama za kujenga muundomsingi siku za baadaye.
- Kuimarisha usimamizi wa data ili kubainisha mchango wa washikadau katika sekta ya ujenzi wa nyumba wakiwemo watakaonufaika na mradi huo.
- Kuanza kutumia teknolojia ya ujenzi wa nyumba ambayo inahifadhi mazingira huku ikipunguza gharama za ujenzi.
- Kuanzisha benki za ardhi na kuboresha mfanyiko tendani wa kanuni.
- Kuimarisha ushirikiano kati ya mashirika ya umma na ya watu binafsi na kutoa vivutio kwa benki za kibiashara, mashirika ya akiba na mikopo, mashirika ya pensheni, bima na pesa zinazotumwa na Wakenya wanaoishi ng'ambo ili kusaidia uhamasishaji wa rasilmali itakayotumiwa kujenga nyumba zinazomudika.
- Kuanza kutumia teknolojia yenye gharama ya chini katika uzalishaji umeme na nishati ili kuhakikisha kuwa bei ya stima ina ushindani wa kuhimili shughuli za kiuchumi.
- Kushughulikia matamanio ya washikadau kwa heshima kuhusiana na matumaini

ya ugunduzi, utoaji na uuzaji wa mafuta na uwezo wa kiuchumi wa kudumu na muungano wa kijamii.

- Kuboresha usimamizi wa rasilmali ya maji na uhifadhi wa vianzo vya maji ili kuhakikisha upatikanaji wa maji pamoja na uwekezaji zaidi katika uvunaji maji, uhifadhi na usambazaji maji (uunganishaji).
- Kuanzisha utaratibu wa kutoa vichocheo kwa sekta ya kibinafsi kuwekeza katika utaratibu wa kuondoa maji machafu.
- Kuwekeza katika elimu ya kidijitali na kuimarisha uvumbuzi ili kuweza kunufaika kutokana na utandawazi ulio na uwezo mkubwa.
- Kuhimiza uwekezaji mwingi zaidi katika simu tamba, utangazaji kupitia mtandao, na huduma za mawasiliano ili kuzidisha mchango wa sekta ya utandawazi kwa uchumi.

## Kuwekeza katika kuwawezesha binadamu

Ili kuzidisha utoaji wa huduma za afya, kuongezea usajili na kubakia shuleni, na kuwalinda wanajamii walio katari ya kudhuriwa, ni muhimu:

- Kuendeleza ushirikiano na sekta ya kibinafsi katika usambazaji wa bima ya afya hasa katika sekta isiyo rasmi. Hii ni muhimu zaidi katika kupunguza malipo ya moja kwa moja.
- Kuwekeza katika ujenzi wa vituo vya afya na rasilmali ya binadamu ili kutimiza viwango vya shirika la afya ulimwenguni (WHO).
- Kuhimiza usuluhishaji wa migogoro ya wafanyikazi wa afya kwa amani.
- Kuongezea ruzuku kwa elimu ya bure katika shule za msingi na shule za upili zisizo za malazi ili kuwapunguzia mzigo wazazi.
- Kuhakikisha ruzuku kwa shule inatumiwa ipasavyo na walimu wakuu ili kupata matokeo ya kielimu.
- Kuanzisha mfumo ufaao wa usimamizi na wa kutathmini ili kuzidisha usimamizi wa wahusika wa ulinzi wa jamii na kuhakikisha kuwa kuna ulinzi wa jamii wa kutosha, wenye ufanisi, na wa kufaa katika nchi nzima.
- Kuunda jukwaa la kutambua juhudi mbalimbali za kuilinda jamii na mipango

kwa manufaa ya umma hasa ile inayopatikana katika maeneo ambayo hayafikiki kwa urahisi.

## Kusimamia maendeleo katika uwekezaji

Ili kukuza uwekezaji wa kibinafsi, kuna haja ya:

- Kudumisha msukumo wa kutekeleza ajenda ya marekebisho katika kubuni mazingira yanayowezesha ili kudumisha imani ya soko, kuboresha na kurahisisha shughuli za kufanyia biashara, na kupunguza gharama za kufanyia biashara.
- Kuzidisha ubunaji wa mazingira yanayowezesha kufanyia biashara hususan katika kiwango cha kaunti ili kudumisha ukuaji na maendeleo ya biashara ndogo kabisa, biashara ndogondogo na za wastani kwa kuzidisha uratibu na sera na urazinishaji wa mfumo wa kanuni katika viwango vya serikali kuu na zile za kaunti.
- Kuzidisha ushirikiano kati ya nchi wanachama wa jumuiya ya Afrika Mashariki kusaidia utekelezaji wa miradi inayotarajiwa kujengwa katika maeneo mbalimbali na ambayo inalenga kuboresha mazingira ya kuwekeza kwa wakati unaofaa.
- Kuoanisha kanuni na taratibu za uwekezaji ili kukubalia utumiaji wa nafasi za kuendeleza viwanda na uwekezaji kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi.